# Nyama Pori na Usalama wa Chakula kwenye Maeneo ya Wakimbizi

**Jambiya, G., Milledge, S.A.H. na Hurst, A.**

**Kuainisha maendeleo na uhifadhi hususan kwenye makazi ya Wakimbizi kaskazini magharibi mwa Tanzania ambako umuhimu wa hali ya uhakika wa maisha ya jamii na kupungua kwa idadi ya wanyama pori vina umuhimu wa kutazamwa kwa pamoja**

© TRAFFIC 2008

Tangu mwaka 1993 Tanzania imekuwa mwenyyeji wa makundi kubwa ya wakimbizi duniani na kwa uhakika imekuwa mwenyeji wa kundi kubwa kwa nchini za Afrika. Idadi hii ya wakimbizi ilifikia kilele kwa kuwa na watu 800,000 lakini kwa sasa imekuwa ikipungua na kufikia kiasi cha watu nusu milioni. Tanzania pia ni nchi mojawapo duniani ambayo ina utajiri mkubwa sana wa raslimali, wanyama pori wengi sana na bioanuwai.Kuwepo kwa idadi kubwa ya wakimbizi karibu na wanyama pori kumesababisha kuwapo na athari kubwa kwa uhifadhi.



Simon Milledge / TRAFFIC

Tanzania ni mwenyeji wa kundi kubwa la wakimbizi Africa, takriban 548,000 ambao theluthi mbili wanaishi katika kambi rasmi za wakimbizi

Kwa kulenga maeneo ya kaskazini magharibi mwa Tanzania, utafiti uliofanywa hivi karibuni na TRAFFIC lilikuwa jaribio la kwanza kutaka kufahamu uwiano uliopo kati ya uhifadhi na matokeo ya matumizi ya nyama pori katika hali ya ukimbizi. Matokeo ya utafiti huu yameshauri yawepo mambo yanayohusu sera na programu mbalimbali yanayolenga kutoa jibu la vishawishi vya matumizi ya nyama pori.Kwa mtazamo wa wigo mpana zaidi kuna uwezekano wa kuwa na uwiano kati ya kuwa na usalama wa chakula na njia za kujipatia riziki kwa wote-wakimbizi na wananchi wakati huo pia kuhakikisha utulivu wa idadi ya wanyama walioko pembezoni mwa jamii husika.

**Mahitaji ya nyama pori kwa upande mmoja yanatokana na mgao mdogo wa chakula kwa wakimbizi ambacho hakina protein ya nyama.**

**Wakimbizi kutuhumiwa kwa kutafuta kile kinachochukuliwa kuwa ni cha muhimu kwa sehemu ya lishe yao ya asili.**

**Uvunaji haramu na biashara ya nyama pori vimesababisha kupungua sana kwa wanyama na kupotea kwa fursa za maendeleo Tanzania.**

## Kupungua sana kwa wanyama pori

Mahitaji ya nyama pori yamesababisha idadi ya wanyama pori kuporomoka ghafla kwenye maeneo yanayozunguka kambi za wakimbizi. Chini ya mwaka mmoja wa wimbi kubwa la wakimbizi kuingia Kagera kuanzia katikati ya mwaka 1994 uwindaji haramu uliongezeka kwa kasi kubwa. Imekadiriwa kwamba kiasi cha tani 7.5 ya nyama pori ikiwa ni sawa na wanyama pori 60 wameuawa bila kibali kila juma na kugawiwa kwenye kambi kubwa mbili za Benaco na Mlima Kilale zenye jumla ya wakimbizi wanaokadiriwa kuwa 450,000.

Ulinganishi wa tafiti za wanyama pori zilizofanywa unaonesha kwamba baadhi ya aina ya wanyama pori zimepungua kwa kati ya asilimia 60 – 90 kwenye maeneo yaliyohifadhiwa kati ya mwaka 1990 na 1998. Wanyama wakubwa wenye kula majani kama nyati, pofu na palahala kwenye pori la hifadhi la Burigi na Biharamulo wamepungua.

Kwenye pori la hifadhi ya Muyowosi na Kigosi baadhi ya aina za wanyama waliopungua zimetambuliwa kuwa ni pamoja na viboko, punda milia na korongo. Maelezo yote kwa ujumba yanaonyesha kwamba kupungua huku kumesababishwa na uwindaji wa wanyama pori usio halali.

Katika hifadhi ya wanyama pori ya Gombe, idadi ya wanyama kama nyati, punda milia, pongo na mindi inaonyesha wamepungua. Takwimu zilizopo zinaonyesha kupungua pia kwa idadi ya sokwe katika hifadhi ya Gombe upande wa kusini mwa hifadhi ambako ndiko penye idadi kubwa ya wahamiaji kutoka Kongo ambao kwa jadi hula nyama ya mnyama huyo.

Uwindaji haramu wa nyama pori umesababisha idadi ya Sokwe katika hifadhi ya Gombe kupungua kwa kasi



© Martin Gunther / WWF-Canon

1 Jambiya, G., Milledge, S. na Tango, N. (2007). ‘Mchicha wa Usiku’: Uhifadhi na madhara ya riziki yatokanayo na matumizi ya nyama pori katika hali ya ukimbizi Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania. TRAFFIC East/Southern Africa, Dar es Salaam, Tanzania. ISBN: 978-1-85850-231-1

# Matokeo muhimu

**Mambo matatu ya kisera yanayohusiana na kushuka kwa idadi ya wanyama na athari zake yanahusiana na usimamizi wa kambi za wakimbizi:**

## Mahitaji ya nyama pori yamekuwa yakiongezeka kutokana na mgao mdogo wa chakula wanaopata

Msukumo mkubwa uliopo katika matumizi ya nyama pori na biashara yake yanatokana na hali ya kutokuwa na usalama wa chakula ambao unatokana na mgao mdogo wa chakula kwa wakimbizi na kukosekana kwa protini itokanayo na nyama. Pamoja na juhudi zinazofanywa na Shirika la Chakula Duniani na washirika wake, kiasi cha chini cha kalori kinachohitajika kwa siku, (2100), hakijaweza kufikiwa kila mara kutokana na utaratibu hafifu wa ugavi au kutokuwepo kwa ufadhili kifedha. Upungufu wa chakula umesababisha mgao kushuka na kufikia kalori 1,400 kwa mkimbizi kwa siku. Zaidi ya hayo mgao huo hauna nyama ambayo kiasili na kimila ni sehemu ya lishe ya Kiafrika.

Kutokana na matatizo ya kisera na kiuchumi yaliyopo, ni wakimbizi wachache sana wanaruhusiwa kufuga mifugo kama mbuzi, nguruwe na kuku kwa ajili ya matumizi ya nyumbani au biashara. Wakimbizi wanajinusuru katika hali hii kwa njia tofauti zikiwepo za wizi, kubadilisha au kuuza mgao wao wa chakula au kuzamia nchini. Njia nyingine wanazotumia kuhakikisha wanakuwa na chakula ni kwenda kando kando ya kambi na kuwinda kwa ajili ya nyama pori kama chakula au kuanzisha mtandao wa uwindaji haramu na kufanya biashara ya nyama pori kwa kushirikiana na wenyeji ambao wana uhuru wa kutoka eneo moja hadi jingine na kusambaza nyama pori.

## Wakimbizi wanatuhumiwa isivyo halali kwa kutafuta chakula ambacho ni haki ya msingi kwa kila binadamu

Utumiaji haramu wa nyama pori unamaanisha kuwa kuhusika na kuwepo mara kwa mara kwa kunaimarisha kuwepo kwa chuki kwa wazawa, hasa upande wa mamlaka za serikali. Ni kweli pia kwamba wazawa wenyewe kwa wakati mwingine kwa kushirkiana na wakimbizi wanafanya biashara na kula nyama pori kutoka vyanzo visivyo halali.

Wakati matukio ya uhalifu yanaonyesha kwamba yapo juu kwenye maeneo ya wakimbizi, takwimu za magereza zinaonyesha kwamba wazawa wanafanya uhalifu zaidi ya wakimbizi. Hata hivyo, idadi isiyowiana ya wakimbizi wamekamatwa kwa uwindaji haramu. Kwa mfano asilimia 87 ya majangili waliokamatwa katika mkoa wa Kagera katikati ya miaka ya 1990 walikuwa wakimbizi.

Kwa pamoja takwimu hizi zinaonyesha kwamba wakimbizi wamekuwa na wanaendelea kuwa watuhumiwa kwa kuendelea kutafuta kile kinachochukuliwa kuwa mahitaji yao muhimu na ya msingi ya chakula. Kwa kiasi fulani wakimbizi wamekuwa wakipata adhabu mara mbili, kwanza mahitaji yao ya msingi ya chakula hayatoshelezi na pili juhudi zao za kupata mahitaji hayo ya msingi zinaonekana ni kinyume cha sheria na kukosa njia halali na mbadala za kuyapata mahitaji hayo.

## Kupungua kwa wanyama na uharamu wa utumiaji nyama pori husababisha kupotea kwa fursa za maendeleo

Hapa nchini, kupungua kwa wanyama pori kunawakilisha kupotea kwa fursa ya mapato yanayotokana na wanyama pori kwa serikali na jamii. Katika mkoa wa Kagera kwa mfano, mapato yatokanayo na uwindaji wa nyara ni faida halisi ya kifedha ambayo serikali inapata. Kutokana na uwindaji haramu idadi ya wanyama imepungua na kusababisha kupungua kwa mapato ya serikali kwa zaidi ya mara nne kati ya mwaka 1991 na 1996 ikionyesha mwelekeo hasi.

Hata hivyo kuna upande mwingine wa suala lenyewe. Jamii ya Watanzania wenyewe wamehusika katika kuvuna na kuuza nyama pori kwa wakimbizi. Kwa sehemu ya nchi ambayo njia mbadala za kupata kipato ni chache, kipato kitokanacho na biashara ya nyama pori bila shaka kimekuwa cha faida kubwa sana hivyo kisipuuzwe. Wakati huohuo, uharamu wa biashara hii umezizuia mamlaka za serikali kudhibiti na kupata mapato yatokanayo na biashara hiyo. Zaidi ya hayo kutokuwepo na wadau wa usimamizi na utumiaji wa raslimali za asili imeonyesha kwamba Watanzania wa kawaida wana motisha kidogo sana wa kushiriki katika kulinda raslimami hizi na badala yake kila mtu kwa nafasi yake amekuwa anazitumia kwa njia ambazo si endelevu.



Watanzania karibu na kambi ya wakimbizi Lugufu wakijiandaa kwenda kuwinda

Simon Milledge / TRAFFIC

# Mapendekezo

Kutokana na kurudishwa kwa wakimbizi wengi Rwanda, kiasi cha biashara ya nyama pori maeneo ya wakimbizi kwa uhakika kimeshuka tangu katikati ya miaka ya 1990. Hata hivyo kambi zilizobaki zimeendelea kuwa tishio kwa idadi ya wanyama. Sababu mbalimbali za matumizi ya nyama pori mikoa ya Kagera na Kigoma yanaonyesha kuhitajika kuwepo muitikio wa sera mbalimbali juu ya hali hii kwa vile njia moja pekee haina matumaini ya kutoa suluhisho la matatizo yanayosababisha na kushawishi matumizi ya nyama pori maeneo ya wakimbizi. Jenasi nne za mapendekezo zimetolewa kupunguza athari hizo:

## Njia tofauti na himasheria zibuniwe na zijaribiwe

Kutokana na jinsi biashara haramu ya nyama pori ilivyo, himasheria na mbinu nyingine za kuongeza uwezo wa usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa ni mbinu kubwa ambazo zimekuwa zikitumiwa na serikali hadi sasa. Utumiaji wa himasheria kulinda wanyama pori itaendelea kuwa nyenzo muhimu kutumika, na hasa kwa wanyama walio hatarini kutoweka kama vile sokwe na tembo. Hata hivyo njia mbadala za kutumia sheria zina upungufu wake na zinaweza kuwa si sawa kila mara. Zaidi ya hapo mbinu ya namna hii haionyeshi kulinda wanyama pori waliosalia kwa mafanikio makubwa.

Pamoja na kutumia sheria, matumizi ya mbinu mbali mbali za kudhibiti biashara ya nyama pori zikiwemo kutoa motisha ambazo zinakubalika kwa jamii na ambazo ni bora kiuchumi na pengine kuleta tija kwao na kutatua tatizo lenyewe la chakula sambamba na uhifadhi na madhara ya utafutaji riziki.

### Ramani ya eneo la utafiti




Tanzania, ikionyesha eneo la utafiti kaskazini-magharibi katika kisanduku

Kwanza uwezekano wa kuwa na biashara ya nyama pori halali, inayoweza kudhibitiwa hata ikiwezekana kwa msimu na maeneo fulani utazamwe. Sera ya wanyama pori inatoa fursa ya namna hii na kuanzishwa kwa maeneo ya jamii ya wanyama pori (WMA) inaweza kuwa ni sehemu nzuri ya kutoa msukumo kushirikisha jamii katika usimamizi wa raslimali ya wanyama pori. Zaidi ya hayo aina ya wanyama kama nguruwe mwitu, pongo na mindi wanaweza kustahimili shinikizo la uwindaji na wangeweza kuwa ndio wanyama wa kuanzia kwa uwindaji endelevu.

Pili, utafiti ufanyike kuangalia uwezekano wa kuwa na ranchi au uendelezaji wa aina fulani ya wanyama pori hususan kwa ajili ya kupata nyama kaskazini magharibi mwa Tanzania kwa serikali kushirikiana na wadau wa maendeleo na jamii inayohusika na uhifadhi kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa nyama ndani ya kambi za wakimbizi.

Tatu, ni vyema busara ikatumika kuhamasisha shughuli za uzalishaji mali mashambani na zisizo za mashambani kwa wananchi na wakimbizi kwa ajili ya kuongeza vipato vyao katika familia. Kuongezeka kwa kipato cha ziada kutawawezesha kununua nyama ya ng'ombe na kupunguza utegemezi wa mahitaji ya nyama pori.




Simon Milledge / TRAFFIC

Watoto waliozaliwa katika kambi za wakimbizi wakisubiri kuondoka kurudi makwao

## Usimamizi wa kambi za wakimbizi hauna budi kuzingatia athari mbaya zitokanazo na kambi hizo kwa mazingira ya wanyama pori na makazi yao ya asili

Wakati Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR) na wadau watekelezaji wenzake wamepata mafundisho mengi yahusianayo na mazingira, mtazamo wa ziada unatakiwa kuelekezwa kwenye mambo yanayohusu wanyama pori kuku msukumo zaidi ukielekezwa katika usimamizi wa kambi za wakimbizi Afrika. Kwa sasa sera ya "usiulize, usiseme" inatekelezwa kila mahali kwenye kambi za wakimbizi magharibi mwa Tanzania wakipuuza nafasi muhimu ya wanyama pori katika kuchangia lishe yao na vilevile athari mbaya zitokanazo na uhifadhi.

Wakati wa awamu ya muitikio wa matatizo yanayokumba ubinadamu, suala la nyama pori lichukuliwe kama sehemu ya mpango wa dharura wa majanga ya wakimbizi na mlolongo mwingine wa hifadhi ya mazingira. Usimamizi na tathmini ya mazingira vikiwemo ukusanyaji wa taarifa za msingi, biashara na matumizi ya nyama pori ni vyema vikahusishwa. Vipimo vya usimamizi ni sharti vitoe taswira ya idadi ya wanyama pori na takwimu za mapato yatokanayo na wanyama pori pale inapobidi.

Wawakilishi kutoka Sekta ya wanyama pori ni lazima wawe miongoni mwa wakala na waratibu wa utaratibu wa kufanya kazi ili kusaidia kuhakikisha kwamba suala la nyama pori linajadiliwa kwenye kambi za wakimbizi, wilayani na ngazi ya taifa. Maeneo yote yanayofanyiwa ukarabati wa mazingira na mpango wa usimamizi (kwa mfano bustani za majumbani, upandaji miti), hatua za kuhakikisha uhakika wa chakula cha kutosha ziingizwe katika mipango hiyo ili kupunguza ujangili.

Cha muhimu zaidi pia ni kwamba wafadhili wa wakimbizi ambao pia wengi wao wanahamasisha na kuunga mkono uhifadhi na miradi ya usimamizi wa wanyama pori Afrika wajulishwe athari yake pale fedha zao zitakapo kuwa hazikidhi mahitaji ya pale kiasi cha chakula kutotosheleza. Wafadhili wengi tayari wameshajitolea kutoa uangalizi bora japo kwa kiwango cha chini lakini ni vyema wakatambua athari ambazo zinaweza kujitokeza iwapo viwango hivi havitafikiwa.

Wafadhili ni vyema wakatambua pia kwamba kuheshimu mapendeleo ya kiutamaduni ya wakimbizi ni muhimu kwani wakati mwingine wakimbizi huhitaji kupatiwa nyama pori kama sehemu ya lishe yao. Kwa hali hiyo ni muhimu kutambua kwamba misaada ya kibinadamu iliyowahusisha watu waliokimbia makazi yao huko Croatia, Slovania na Serbia mapema miaka ya 1990 kwa mfano, iliendana na kutoa protini ya nyama kila mara.

Mahali pa kuweka kambi za wakimbizi ni suala jingine la muhimu kuangalia. Ushauri kutoka mamlaka za wanyama pori ni muhimu wakati kambi mpya za wakimbizi zinapoanzishwa, zinapofungwa au kuimarisha kambi zilizoko.

## Usimamizi fasaha dhidi ya matumizi ya nyama pori sharti uhusishe wahifadhi na watoa misaada ya kibinadamu

Zaidi ya uelewa, kuna haja ya wazi ya mpango wa wadau kuruhusu ushauri maalamu wa kitaalam kutoka kwa jamii ya wahifadhi kuunganishwa na mpango wa muda mrefu wa maendeleo ya jamii.

Kwa mtazamo wa hali ya mazingira ya kambi za wakimbizi, ni muhimu kwa makundi ya asasi za kiraia za ndani zinazoshughulika na mambo ya mazingira kuingia kwenye mazungumzo na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani na wadau wengine muhimu ili kujadiliana na kukubaliana njia bora ya kushughulikia suala la nyama pori kwa kuzingatia mpango wa kukuza uchumi na kuondoa umasikini Tanzania (MKUKUTA). Njia mbili muhimu za kuanzisha mazungumzo ni pamoja na kuanzisha mjadala wa kila mwezi ya mashirika-wadau na wadau wadogo wa maendeleo juu ya masuala yanayohusu wakimbizi.

**Uvunaji usiyo endelevu wa nyama pori kwenye maeneo ya wakimbizi kaskazini magharibi mwa Tanzania ni tatizo kubwa ambalo halijapewa kipaumbele inachokistahili. Ni wachache wanatambua umuhimu wa lishe, afya na kipato kwa manufaa ya wakimbizi wakati huo huo wengine wakitambua umuhimu wa muda mrefu wa athari kiuchumi na kimazingira kwa uvunaji usio endelevu.**

**Matumizi bora ya sheria na kanuni za hifadhi ya wanyama pori haviwezi kutoa suluhisho la visababishi vya matumizi haramu ya nyama pori. Motisha chanya kupitia mfumo uliosawa wa biashara ya nyama pori au utoaji njia mbadala za upatikanaji wa protini au njia mbadala za kuboresha maisha ya wahusika ndizo ambazo zingeweza tu kukidhi matakwa ya wakimbizi na maendeleo muhimu ya jamii kwa ujumla.**

**Wadau wote, watunga sera na wale wanaosaidia taasisi za wakimbizi na mameneja wa wanyama pori ni vyema wakapanua wigo wa kuzitazama na kuzikubali sera na programu ambazo zitakidhi mahitaji ya kuweza kupunguza matumizi ya nyama pori yasiyo endelevu.**

**This project is part of TRAFFIC's wild meat programme in East and southern Africa funded by:**

Sida

The Rufford Maurice Laing Foundation

WWF for a living planet

TRAFFIC the wildlife trade monitoring network is a joint programme of WWF IUCN The World Conservation Union

**www.traffic.org**

Layout and design by Richard Thomas

TRAFFIC is a UK registered charity No. 1076722